TANGAZO LA SERIKALI NA. 550 la tarehe 4/8/2023

SHERIA YA NGUVU ZA ATOMU,

(SURA YA 188)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 70)*

KANUNI ZA NGUVU ZA ATOMU ZA UDHIBITI WA MIONZI KATIKA MNYORORO WA VYAKULA NA BIDHAA ZINAZOHUSIANA NA CHAKULA, ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MATAKWA YA KUPATA CHETI CHA UCHUNGUZI WA MIONZI

4. Uchunguzi wa uchafuzi wa mionzi.
5. Uondoshaji wa bidhaa za mnyororo wa chakula na bidhaa zinazohusiana na chakula.
6. Uchukuaji wa sampuli.
7. Zuio la kuingiza bidhaa nchini, kusafirisha bidhaa nje ya nchi, kuzalisha au kusambaza bidhaa katika mnyororo wa chakula na bidhaa zinazohusiana na chakula zilizochafuliwa kwa mionzi.
8. Katazo kuhusu matumizi ya visima na hifadhi za maji
9. Cheti au leseni ya uchunguzi wa mionzi.

10. Ada.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA JUMLA

11. Wajibu wa kuzingatia maelekezo ya Tume.
12. Makosa na adhabu.
13. Kufutwa kwa Kanuni.

MAJEDWALI

SHERIA YA NGUVU ZA ATOMU,
(SURA YA 188)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 70)*

# KANUNI ZA NGUVU ZA ATOMU ZA UDHIBITI WA MIONZI KATIKA MNYORORO WA VYAKULA NA BIDHAA ZINAZOHUSIANA NA CHAKULA, ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Nguvu za Atomu za Udhibiti wa Mionzi katika Mnyororo wa Vyakula na Bidhaa Zinazohusiana na Chakula, za mwaka 2023.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika mnyororo wa vyakula vyote na bidhaa zinazohusiana na chakula.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"msafirishaji wa bidhaa nje ya nchi" maana yake ni mtu, kampuni au taasisi yoyote inayopeleka bidhaa nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali ikiwemo biashara au misaada;

"msindikaji" maana yake ni mtu, kampuni au taasisi yoyote inayobadili bidhaa za mnyororo wa chakula kuwa katika aina nyingine ya chakula;

"muingizaji wa bidhaa nchini" maana yake ni mtu, kampuni au taasisi yoyote inayoingiza bidhaa nchini kwa madhumuni mbalimbali ikiwemo

biashara au misaada;

"mzalishaji" maana yake ni mtu, kampuni au taasisi inayotengeneza bidhaa katika mnyororo wa chakula isipokuwa mkulima na mzalishaji wa mbegu;

Sura ya 188

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Nguvu za Atomu;

"Tume" maana yake ni Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria;

"vyakula vya wanyama" maana yake ni vyakula vilivyokusudiwa kwa ajili ya mifugo;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala yanayohusiana na nguvu za atomu.

## SEHEMU YA PILI
## MATAKWA YA KUPATA CHETI CHA UCHUNGUZI WA MIONZI

Uchunguzi wa uchafuzi wa mionzi

4. Mtu hataingiza nchini, hataondosha kupitia forodha au kusambaza, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani au kama chakula cha wanyama, bidhaa yoyote iliyoorodheshwa katika Jedwali la Kwanza, isipokuwa kama-

(a) uchunguzi wa mionzi chini ya Sheria hii umefanyika kwenye bidhaa hiyo; na

(b) leseni au cheti kimetolewa kuthibitisha kuwa bidhaa hiyo ni salama au ina uchafuzi wa mionzi ulio chini ya ukomo ulioainishwa katika Jedwali la Pili.

Uondoshaji wa bidhaa za mnyororo wa chakula na bidhaa zinazohusiana na chakula

5. Kwa kuzingatia kifungu cha 30 cha Sheria, mtu yeyote ambaye ataingiza nchini au kusafirisha kwenda nje ya nchi bidhaa zozote za vyakula zilizoainishwa katika Jedwali la Kwanza atatoa cheti cha uchunguzi wa mionzi kwa kila shehena kabla ya uondoshaji kwa ajili ya kuingizwa au kutolewa kupitia forodha kama itakavyohitajika na uondoshaji kupita forodha hautafanyika isipokuwa kama cheti cha uchunguzi wa mionzi ya bidhaa

husika kimetolewa.

Uchukuaji wa sampuli

6.-(1) Msafirishaji bidhaa nje ya nchi, muingizaji bidhaa nchini, msambazaji, mzalishaji au msindikaji au mfadhili ikijumuisha idara za Serikali kama itakavyohitajika atatakiwa kuruhusu uchukuaji wa sampuli ya kutosha kutoka kwenye bidhaa zilizoainishwa ambazo zinakusudiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi au kuingizwa nchini, au kusambazwa.

(2) Uchukuaji wa sampuli wa bidhaa chini ya Kanuni hizi utafanywa kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa na Tume.

Zuio la kuingiza bidhaa nchini, kusafirisha bidhaa nje ya nchi, au kusambaza bidhaa katika mnyororo wa chakula na bidhaa zinazohusiana na chakula zilizochafuliwa kwa mionzi

7.-(1) Tume itarudisha bidhaa zilizoainishwa katika Jedwali la Kwanza zinazoingizwa nchini zikiwa zimechafuliwa na mionzi kwa kiwango kinachozidi kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Pili katika nchi zilikotoka kwa gharama za mwingizaji.

(2) Endapo baada ya uchunguzi bidhaa yoyote ya mnyororo wa chakula au bidhaa inayohusiana na chakula inayokusudiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi itakutwa imechafuliwa na mionzi kwa kiwango kinachozidi kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Pili, bidhaa hiyo haitasafirishwa kwenda nje nchi na itachukuliwa kama bidhaa ya chakula iliyochafuliwa na mionzi na itaondolewa kwa namna Tume itakavyoainisha.

Katazo kuhusu matumizi ya visima na hifadhi za maji

8.-(1) Mmiliki wa kisima cha maji au hifadhi ya maji hataruhusu kisima au hifadhi kutumika kabla ya uchunguzi wa mionzi kufanywa na Tume.

(2) Kwa upande wa kisima cha maji au hifadhi ya maji iliyokuwa inayumika kabla ya kuanza kwa Kanuni hizi, Tume itaweka utaratibu wa namna ambayo mmiliki wa kisima au hifadhi atawasiliana na Tume kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa uchafuzi wa mionzi wa kisima cha maji au hifadhi ya maji husika.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii, “mmiliki”

hujumuisha mmiliki halisi au mtu mwingine yeyote anayewajibika na usimamizi wa kisima au hifadhi ya maji.

Cheti au leseni ya uchunguzi wa mionzi

9. Baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa mionzi chini ya kanuni ya 4 na kujiridhisha kuwa bidhaa husika imekidhi viwango, Tume itatoa leseni au cheti cha uchunguzi wa mionzi kwa utaratibu ulioainishwa katika miongozo ya Tume.

Ada

TS. Na 478 la mwaka 2022

10. Tume itatoza ada kwa huduma inazotoa kuhusiana na uchunguzi wa uchafuzi wa mionzi chini ya kanuni hizi kwa viwango vilivyoainishwa katika Kanuni za Ada na Tozo:

Isipokuwa, Tume inaweza kuainisha ada tofauti kuhusiana na bidhaa katika mnyororo wa vyakula au bidhaa zinazohusiana na chakula zilizokusudiwa kwa ajili ya misaada.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA

Wajibu wa kuzingatia maelekezo ya Tume

11. Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madhumuni ya Kanuni hizi, msafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi, muingizaji wa bidhaa nchini msambazaji, mzalishaji au msindikaji wa bidhaa zozote zilizoainishwa au mmiliki wa kisima au hifadhi ya maji atazingatia maelekezo yaliyotolewa na Tume katika utekelezaji wa mamlaka yake chini ya Kanuni hizi.

Makosa na adhabu

12. Mtu yeyote, ambaye atakiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu zilizoainishwa katika Sheria.

Kufutwa kwa Kanuni TS Na. 63 la mwaka 1998.

13. Kanuni za Kinga dhidi ya Mionzi za Udhibiti wa Bidhaa za Vyakula Zilizochafuliwa na Mionzi, za mwaka 1998 zimefutwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4)*

1. Maziwa (aina zote za maziwa na bidhaa za maziwa)
2. Nyama (aina zote za nyama na bidhaa za nyama)
3. Samaki (aina zote za samaki na vyakula vinavyopatikana kwenye maji)
4. Mbogamboga na mafuta ya mboga
5. Matunda na bidhaa za matunda
6. Ngano na bidhaa za ngano
7. Chai
8. Mchele
9. Uyoga
10. Tumbaku na bidhaa zake kwa matumizi ya binadamu
11. Vyakula vya wanyama vya aina zote
12. Maji (Aina zote za maji ikijumuisha maji ya visima na hifadhi ya maji)
13. Sigara
14. Aina zote za vinywaji
15. Maharagwe na jamii zote za kunde
16. Mahindi, bidhaa zote za mahindi na nafaka
17. Kawaha na bidhaa za kahawa
18. Mbolea
19. Biskuti, chokoleti na pipi
20. Shayiri na bidhaa za shayiri
21. Vyakula cha watoto wachanga
22. Chumvi na Sukari
23. Viungo vya chakula
24. Mbegu za aina zote
25. Virutubisho vya vyakula
26. Bidhaa za vyakula zenye matumizi zaidi ya moja
27. Aina zote za vyakula na bidhaa zinazohusiana na chakula kwenye mnyororo wa vyakula

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4)*

**Ukomo wa udhibiti wa bidhaa za mnyororo wa chakula na bidhaa zinazohusiana na chakula**

Viwango vya Viasili vya mionzi vinavyotoa mionzi ya beta/gama: Bq/kg or Bg/l viwango vya aktinaidi

**A: Ukomo wa udhibiti wa visiali vya mionzi kwenye mnyororo wa chakul**

| Jina la Bidhaa | Viasili vya Mionzi | Ukomo (Bq/kg) |
|---|---|---|
| Vyakula vya watoto wachanga* (Vyakula vinavyokusudiwa kwa ajili ya matumizi ya watoto wachanga) | $^{238}$Pu, $^{239}$Pu, $^{240}$Pu, $^{241}$Am | 1 |
| | $^{90}$Sr, $^{106}$Ru, $^{129}$I, $^{131}$I, $^{235}$U | 100 |
| | $^{35}$S$^{**}$, $^{60}$Co, $^{89}$Sr, $^{103}$Ru, $^{134}$Cs, $^{137}$Cs, $^{144}$Ce, $^{192}$Ir | 1000 |
| | $^{3}$H$^{***}$, $^{14}$C, $^{99}$Tc | 1000 |
| Vyakula vingine visivyo vya watoto wachanga | $^{238}$Pu, $^{239}$Pu, $^{240}$Pu, $^{241}$Am | 10 |
| | $^{90}$Sr, $^{106}$Ru, $^{129}$I, $^{131}$I, $^{235}$U | 100 |
| | $^{35}$S$^{**}$, $^{60}$Co, $^{89}$Sr, $^{103}$Ru, $^{134}$Cs, $^{137}$Cs, $^{144}$Ce, $^{192}$Ir | 1000 |
| | $^{3}$H$^{***}$, $^{14}$C, $^{99}$Tc | 10000 |

**B: Ukomo wa udhibiti wa viasili vya mionzi kwenye maji ya kunywa**

| Viasili vya mionzi* | Ukomo (Bq/l) |
|---|---|
| $^{3}$H | 10000 |
| $^{14}$C$^{**}$ | 100 |
| $^{90}$Sr, $^{131}$I, $^{134}$Cs, $^{137}$Cs,$^{238}$U$^{***}$ | 10 |
| $^{226}$Ra, $^{228}$Th, $^{230}$Th, $^{232}$Th,$^{234}$U, $^{239}$Pu, $^{241}$Am, | 1 |
| $^{210}$Pb, $^{210}$Po, $^{228}$Ra | 0.1 |

Ukomo uliopo hapo juu utatumika isipokuwa wakati wa dharura za majanga ya kiradiolojia ambapo ukomo ulioanishwa na Tume utatumika.

Dodoma,
27 May, 2023

ADOLF F. MKENDA
*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia,*